



## **TAARIFA KWA UMMA**

Kuna taarifa zinazotumwa kwa wananchi kwa njia ya simu zikidai kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF una nafasi za kazi kwa ajili ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Taarifa hizi zimekuwa zikiwataka wanaohitaji ajira hizo kutoa fedha ili kupata ajira hizo.

Ajira za muda ni utaratibu unaotumika katika utekelezaji wa shughuli za Mpango na unawahusu WALENGWA wa Mpango ambao TASAF ina orodha yao. Hawahitajiki kujiandikisha mahali pengine popote wala kutoa fedha ili kupata ajira hizo.

Wananchi wanatakiwa kupuuza taarifa hizo kwani ni za upotoshaji na wanaosambaza taarifa hizo wanafanya hivyo kwa maslahi yao binafsi. TASAF haihusiki na taarifa hizo.